


# Jinsi ya kutumia kondomu ya kike ya FC2

Maelekezo haya yanaonyesha hatua kwa hatua jinsi ya kuingiza kondomu ya kike ya FC2 ndani ya uke. FC2 inaweza kuingizwa ama masaa machache au kabla tu ya kujamiiana. Wakati FC2 inatumiwa kwa mara ya kwanza, watu wanaweza kuhitaji mazoezi ya kuingiza. FC2 inaweza kuingizwa na wanawake wenyewe lakini wenzi wao wanaweza pia kuwaingizia.



**1** Kabla ya kufungua FC2 yako:

- Angalia tarehe ya kuisha muda wa matumizi ambayo imegongwa kwa muhuri mbele au kwenye upande wa pakiti ya FC2.
- Sambaza kilainishi ndani kuzunguka kwa kusugua pakiti kwa mikono yako.


**2**

- Ili kufungua pakiti, chana moja kwa moja kutoka kwenye mshale hapo juu kisha utoe kondomu.
- Usitumie mkasi, kisu au meno yako kufungua pakiti.




**3**

Shika pete ya ndani kati ya kidole gumba chako na kidole cha mbele. Kisha bonyeza pembe za pete ya ndani pamoja ili kutengeneza uimara.



**4**

Unaweza kuingiza FC2 kwa njia nyingi tofauti. Tafuta mkao wa starehe. Hii inaweza kuwa kusimama, kukaa, kuchuchumaa au kulala chini.




**5**

Gusa mashavu ya nje ya uke wako na uyapanue.


Kondomu ya Kike ya FC2 inatengenezwa na The Female Health Company (FHC).  
Chicago USA/London UK/Malaysia






6

- Tumia upande wa pete ya ndani uliobonyezwa kusukuma FC2 kuingia ukenu mwako.
- Sogeza kidole cha kwanza au cha kati ndani ya kondomu na sukuma ndani ya uke wako mbali kadri uwezavyo, kwa kutumia pete ya ndani.
- Hakikisha kondomu haijazungushwa na imekaa vizuri dhidi ya kuta za uke wako.



7

Sehemu ndogo ya kondomu, ikiwemo pete ya nje, inakaa nje ya mwili wako na iko juu ya mashavu ya uke wako, kwa sehemu inalinda viungo vyako vya nje vya kujamiiana na kufunika sehemu ya chini ya uume wa mwenzi wako.




8

FC2 huingia ndani sambamba na uke wako na kuziba shingo ya kizazi. Shingo ya kizazi chako ni ndogo sana kiasi kwamba haiwezekani FC2 kupenya eneo hili.



9


Shika pete ya nje wakati mwenzi wako anapoingiza uume wake ndani ya kondomu. Uume wake ukishaingia ndani ya kondomu, sio lazima uendelea kushikilia pete ya nje. Kwa raha ya ziada unaweza kutaka kuongeza kilainishi zaidi ndani au nje ya FC2 au moja kwa moja kwenye uume wa mwenzi wako mara tu kondomu baada ya kondomu kuingiwa.



10

**Tafadhali zingatia!** Mwenzi wako anatakiwa kuchomoa uume wake mara moja endapo:

- Uume wake utaingia kati ya kondomu na kuta za uke. Hili likitokea unapaswa kurudisha pete ya nje katika nafasi yake kabla hajaingiza tena uume wake ndani ya kondomu.
- Pete ya nje itakua imesukumwa ndani ya uke wako. Hili likitokea unapaswa kutumia FC2 mpya.



11

Kutoa FC2, shika pete ya nje na izungushe kuzuia shahawa kumwagika. Ni vyema ufanye hivi kabla haujasimama. Vuta kondomu nje polepole, ifunge kwenye tishu au pakiti tupu, na kisha itupe kwenye ndoo ya uchafu.



[www.fc2femalecondom.com](http://www.fc2femalecondom.com)

[info@fc2femalecondom.com](mailto:info@fc2femalecondom.com)

f @FemaleCondomFC2

t FC2FemaleCondom

v FC2FemaleCondom